

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

MKOA WA RUKWA
Anuani ya Simu: "REGCOM"
Simu Na: 025-2802318/2802137
Nukushi. (025) 2802217
Barua pepe: ras@rukwa.go.tz



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
1 Barabara ya Mkoani,
S.L.P. 128,
55180 Sumbawanga,
RUKWA.

TAARIFA KWA UMMA

MITIHANI YA UPIMAJI DARASA LA NNE 2023

Kuanzia tarehe **25 Oktoba 2023** wanafunzi wa darasa la nne nchini kote wataanza mitihani ya upimaji ambao inatarajiwa kukamilika tarehe **26 Oktoba 2023**.

Katika Mkoa wa Rukwa jumla ya watahiniwa **41,471** wataungana na watahiniwa wengine nchini kufanya mitihani huo wa darasa la nne.

Ambapo jumla ya watahiniwa **41,471** kati yao wasichana ni **22,164** na wavulana ni **19,307**.

Jumla ya vituo vya kufanyia mitihani ni **386** ikiwa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga ina Vituo **70**, Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ina Vituo **105**, Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ina Vituo **98** na Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ina Vituo **113**.

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Rukwa inawatakiwa kila la kheri wanafunzi wote wa darasa la nne Mkoani Rukwa na Tanzania kwa ujumla katika mitihani yao ya upimaji na kuwaombea wafanye vyema huku wakizingatia taratibu zote za mitihani.

Imetolewa na

Khadija Dalasia

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

Mkoa wa Rukwa

25 Oktoba 2023